# Sheria Ndogo za Kijiji cha Kashagulu

# Usimamizi Shirikishi wa Msitu wa Hifadhi ya Kijiji na Hifadhi ya Mazalia ya Samaki ya Ziwa Tanganyika Sehemu ya Kijiji cha Kashagulu 2007



**SHERIA ZA SERIKALI ZA MITAA**

**(MAMLAKA ZA WILAYA) NA. 7 YA 1982**

**SHERIA NDOGO**

Zimundwa chini ya Kifungu cha 167

# Yaliyomo


1. Jina ........ 1
2. Tarehe ya Kuanza na Eneo la Kutumika kwa Sheria hii. ........ 1
3. Marekebisho ya Sheria ........ 1
4. Tafsiri ........ 2
5. Madhumuni ........ 5
6. Umilikaji ........ 5
8. Kamati ya Mazingira ........ 6
9. Majukumu ya Kamati ya Mazingira ........ 7
10. Ulinzi na Ukaguzi wa Msitu wa Hifadhi ya kijiji na Hifadhi ya Mazalia ya Samaki ya Ziwa Tanganyika Sehemu ya Kijiji cha Kashagulu ........ 9
11. Walinzi wa Msitu wa hifadhi ya kijiji na Hifadhi ya Mazalia ya Samaki ya Ziwa Tanganyika ........ 10
12. Masharti ya Kuingia msitu wa Hifadhi ya Kijiji na Hifadhi ya Mazalia ya Samaki ya Ziwa Tanganyika Sehemu ya Kashagulu. ........ 12
13. Masharti ya Matumizi ya Msitu wa Hifadhi ya Kijiji na Hifadhi ya Mazalia ya Samaki ya Ziwa Tanganyika sehemu ya Kashagulu. ........ 13
14. Vitendo Vilivyopigwa Marufuku ........ 14
15. Vitendo Vinavyoruhusiwa kwa Vibali na Malipo ........ 15
16. Kiasi cha malipo ........ 16
17. Vitendo Vinavyohitaji Kibali bila malipo (Bure) ........ 17
18. Viwango vya Faini ........ 18
19. Gharama na Fidia ........ 20
20. Faini ya wenye Dhamana/ Madaraka ........ 20
21. Taratibu za Kushughulikia Wahalifu wa Msitu wa Hifadhi na Hifadhi ya Mazalia ya Samaki ya Ziwa Tanganyika sehemu ya Kashagulu. ........ 21
22. Namna ya Kushughulikia Mazao ya Msitu na Ziwa Tanganyika Yaliyokamatwa, Faini Zilizotozwa na Mgawanyo Wake: ........ 23
23. Kuwasilisha Mashauri Mahakamani ........ 24
24. Hatua za Mahakamani ........ 24
25. Mapato na Matumizi ya Fedha za Hifadhi ya Msitu na Hifadhi ya Mazalia ya Samaki ya Ziwa Tanganyika Sehemu ya Kijiji cha Kashagulu. ........ 25
26. Matumizi ya Fedha za Kamati ya Mazingira ........ 26

## SHERIA NDOGO

Zimeundwa chini ya Kifungu cha **167**

### 1. Jina

1.1. Sheria ndogo hizi ziitwe"Sheria ndogo za Kijiji cha Kashagulu (Usimamizi Shirikishi wa Msitu wa Hifadhi ya Kijiji na Hifadhi ya Mazalia ya Samaki ya Ziwa Tanganyika Sehemu ya Kijiji cha Kashagulu), 2007"

### 2. Tarehe ya Kuanza na Eneo la Kutumika kwa Sheria hii.

2.1. Sheria hii ndogo ya kijiji itaanza kutumika baada ya kupitishwa na Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma kwa kutiwa sahihi na Mwenyekiti na Mkurugenzi Mtendaji wa Halimashauri ya Wilaya ya Kigoma.

2.2. Sheria hii itatumika ndani ya mipaka ya eneo la Kijiji cha Kashagulu.

### 3. Marekebisho ya Sheria

3.1. Halmashauri ya Kijiji cha Kashagulu kwa idhini ya Mkutano Mkuu wa kijiji inaweza kufanya marekebisho ya Sheria hii bila kuharibu au kukiuka madhumuni ya kimsingi yaliyopelekea kuwepo kwa Sheria hii.Sheria hii itafanyiwa marekebisho na kupitishwa na Mkutano Mkuu wa kijiji na Kamati ya Maendeleo ya Kata ya Kalya.

3.2. Mapendekezo ya mabadiliko yanayokusudiwa kufanywa ni lazima yapelekwe kwa Afisa Misitu/Uvuvi Wilaya kwa ushauri zaidi.

3.3. Taarifa za mabadiliko haya ni lazima zitumwe kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma.

## 4. Tafsiri

4.1. Katika Sheria hii tafsiri zifuatazo zimekusudiwa:

4.1.1. **"Msitu wa Hifadhi ya kijiji"** maana yake ni sehemu ya ardhi ya kijiji yenye msitu iliyotengwa na kuhifadhiwa, ambayo kwa mujibu wa Sheria hii utakuwa Msitu wa Hifadhi ya kijiji cha Kashagulu.

4.1.2. **"Hifadhi ya mazalia ya samaki ya Ziwa Tanganyika"** maana yake ni mita mia (100) ya sehemu ya Ziwa Tanganyika toka kingo za ziwa ambayo ni muhimu kwa mazalia ya samaki.

4.1.3. **"Mpango wa Usimamizi Shirikishi wa Msitu na mazalia ya samaki ya Ziwa Tanganyika"** maana yake ni mpango au utaratibu wa utekelezaji uliotayarishwa na Kamati ya Mazingira ya kijiji kwa ushauri wa wataalam wa misitu na uvuvi kwa lengo la kuelekeza namna ya utekelezaji wa utumiaji, ulinzi, na uendelezaji wa msitu wa hifadhi ya kijiji na hifadhi ya mazalia ya samaki ya Ziwa Tanganyika sehemu ya kijiji cha Kashagulu.

4.1.4. **"Kamati ya Mazingira"** maana yake ni Kamati ya Mazingira ya kijiji cha **Kashagulu** ambayo imepewa jukumu la kusimamia utumiaji, ulinzi na uendelezaji wa msitu wa hifadhi ya kijiji na mazalia ya samaki ya Ziwa Tanganyika sehemu ya Kashagulu.

4.1.5. **"Maeneo yaliyozuiliwa/hifadhiwa"** maana yake ni maeneo yeyote katika msitu wa hifadhi ya kijiji na Ziwa Tanganyika ambayo kutokana na umuhimu wake imeamuliwa na Halmashauri ya kijiji na Kamati ya Mazingira yahifadhiwe /zuiliwe kwa matumizi fulani kwa wakati husika.

4.1.6. **“Maeneo ya matumizi”** maana yake ni yale maeneo ndani ya msitu wa hifadhi ya kijiji cha Kashagulu ambayo Kamati ya Mazingira na Halmashauri ya kijiji imeamua yaruhusiwe kwa matumizi mbali mbali endelevu.

4.1.7. **“Mlinzi/walinzi wa msitu na ziwa”**maana yake ni mtu au watu waliochaguliwa na Mkutano Mkuu wa kijiji/Halmashauri ya kijiji kwa ajili ya kufanya doria za ukaguzi ndani ya eneo la msitu wa hifadhi ya kijiji na mazalia ya samaki ya Ziwa Tanganyika sehemu ya kijiji cha Kashagulu.

4.1.8. **“Halmashauri ya kijiji”**maana yake ni Halmashauri ya kijiji cha Kashagulu.

4.1.9. **“Mkutano Mkuu wa kijiji”** maana yake ni mkutano wa wanakijiji wote wa kijiji cha Kashagulu**.** Huu ndio mkutano wenye mamlaka ya kufanya uamuzi wa masuala yote kijijini.

4.1.10. **“Mahakama”** maana yake ni Mahakama ya Mwanzo au ya Wilaya.

4.1.11. **“Mwenyekiti wa kijiji”** maana yake ni Mwenyekiti wa Halmashauri ya Kijiji cha Kashagulu.

4.1.12. **“Afisa Mtendaji wa kijiji”** maana yake ni Afisa Mtendaji wa kijiji cha Kashagulu

4.1.13. **“Afisa Mtendaji wa Kata”** maana yake ni Afisa Mtendaji wa Kata ya Kalya

4.1.14. **“Mwenyekiti wa kitongoji”** maana yake ni kiongozi aliyechaguliwa kuongoza kitongoji chochote katika kijiji cha Kashagulu.

4.1.15. **“Afisa Misitu Wilaya”** maana yake ni Afisa Misitu wa Serikali anayesimamia na kuongoza

matumizi ya rasilimali ya misitu katika Wilaya ya Kigoma.

4.1.16. **"Kitongoji"** maana yake ni kitongoji chochote cha kijiji cha Kashagulu kinachotambuliwa na Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma.

4.1.17. **"Vyanzo vya maji"** maana yake ni chemchem, mito, makorongo, ardhi oevu katika eneo la msitu wa hifadhi ya kijiji.

4.1.18. **"Miteremko mkali"** maana yake ni ardhi yeyote ndani ya msitu wa hifadhi ya kijiji yenye mwinuko wa nyuzi 30 ($30^0$) au zaidi.

4.1.19. **"Mazao ya misitu" maana** yake ni rasilimali yoyote inayopatikana kutoka msituni kama vile: miti, mbao, kuni, mkaa, fito, nguzo, magome, kamba, unga wa mbao, mizizi, gundi, mbegu, majani, matunda, mboji, udongo, asali, nta na mafuta.

4.1.20. **"Zana"** maana yake ni vifaa vinavyotumika kihalali au isiyohalali kukatia miti na ni pamoja na misumeno, shoka, panga, mundu, kisu, jembe au kifaa kingine chochote kinachoweza kukata mazao ya misitu. Pia vifaa vinavyotumika katika kuvulia samaki majini ikiwa ni pamoja na nyavu, mitumbwi, ndoano na kokoro.

4.1.21. **''Mhalifu"** maana yake ni mtu yeyote atakayekiuka/kuvunja Sheria hizi ndogo, Sheria Kuu ya Misitu No.14, 2002 na Sheria zinazosimamia rasilimali ya Ziwa Tanganyika.

4.1.22. **"Wanyamapori"** maana yake ni jamii ya wanyama wote wanaopatikana na kuishi

kwenye maeneo yao ya asili ndani ya misitu na mapori yanazozunguka msitu wa hifadhi ya kijiji cha Kashagulu. Baadhi ya wanyama hao ni sungura, kongoni, nyati/mbogo, faru, tembo, swala, fisi, chui, mamba, simba, n.k.

## 5. Madhumuni

5.1. Sheria hizi ndogo zimeundwa na Halmashauri ya kijiji na kupitishwa na Mkutano Mkuu wa kijiji kwa lengo / madhumuni ya kutumia, kulinda na kuendeleza eneo la msitu wa hifadhi ya kijiji na hifadhi ya mazalia ya samaki ya Ziwa Tanganyika sehemu ya kijiji cha Kashagulu kwa kuzingatia taratibu zilizoainishwa katika Mpango wa Usimamizi Shirikishi wa Msitu wa Hifadhi ya Kijiji na Hifadhi ya Mazalia ya Samaki ya Ziwa Tanganyika sehemu ya kijiji cha Kashagulu.

5.2. Sheria hizi ndogo zinatoa madaraka kamili kwa Kamati ya Mazingira kwa niaba ya Halmashauri ya kijiji kusimamia matumizi, ulinzi na uendelezaji wa msitu wa hifadhi ya kijiji na hifadhi ya mazalia ya samaki ya Ziwa Tanganyika sehemu ya kijiji cha Kashagulu na itawajibika katika kuthibiti matumizi ya eneo la msitu na ziwa, na kuwashughulikia watu wanaokiuka Sheria hizi.

## 6. Umilikaji

6.1. Eneo la Msitu wa Hifadhi ya kijiji cha Kashagulu linabakia kuwa sehemu kamili ya ardhi ya Halmashauri ya kijiji cha Kashagulu na eneo la hifadhi ya mazalia ya samaki ya Ziwa Tanganyika linabakia kuwa ni mali ya Taifa la Tanzania, hivyo Halmashauri ya kijiji cha Kashagulu itakuwa msimamizi tu kuhakikisha kuwa Ziwa Tanganyika linatumika kwa matumizi endelevu.

## 7. Meneja Mteule

7.1. Mkurugenzi wa Misitu na Nyuki Tanzania ameiteua Halmashauri ya kijiji cha Kashagulu kuwa Meneja Mteule wa msitu wa hifadhi ya kijiji cha Kashagulu.

7.2. Halmashauri ya kijiji cha Kashagulu kwa mujibu wa taratibu za utendaji imeteua Kamati ya Mazingira ya kijiji kutekeleza jukumu la usimamizi wa msitu wa hifadhi ya kijiji na hifadhi ya mazalia ya samaki ya Ziwa Tanganyika kwa niaba yake.

## 8. Kamati ya Mazingira

8.1. Kamati ya Mazingira iliyopendekezwa na serikali ya kijiji na kuidhinishwa na Mkutano Mkuu wa kijiji itakuwa na wajibu wa kutekeleza jukumu la usimamizi wa msitu wa hifadhi ya kijiji na hifadhi ya mazalia ya samaki ya Ziwa Tanganyika chini ya serikali ya kijiji

8.2. Kamati ya Mazingira itachaguliwa kila baada ya miaka mitatu na itakuwa na wajumbe wasiozidi kumi na nne (14) kwa uwakilishi wa kutoka kila kitongoji. Idadi ya wajumbe wanawake isipungue 30% ya wajumbe wote wa Kamati ya Mazingira.

8.3. Kamati ya Mazingira itachagua viongozi wake kutoka miongoni mwa wajumbe wake. Nafasi za uongozi katika Kamati ya Mazingira ni Mwenyekiti, Katibu na Mweka Hazina.Kila mjumbe wa Kamati ya Mazingira anaweza kupewa jukumu maalumu kama watakavyoona inafaa.

8.4. Mabadiliko katika uongozi wa Kamati ya Mazingira yanaweza kufanyika wakati wowote ilimradi uongozi mpya unachaguliwa kwa uwingi wa kura za wajumbe wa Kamati ya Mazingira. Ni lazima Serikali ya Kijiji ijulishwe kuhusu azma ya kufanya mabadiliko hayo.

8.5. Kamati ya Mazingira itakutana mara moja kila mwezi katika hali ya kawaida. Vikaovya dharura vinaweza kufanyika wakati wowote. Vikao vya Kamati ya Mazingira vitafanyika iwapo mahudhurio ya wajumbe wa Kamati ya Mazingira itakuwa zaidi ya nusu ya idadi ya wajumbe. Katibu wa Kamati ya Mazingira ataandika mihtasari ya vikaoyenye nakala kwa Afisa Mtendaji wa Kijiji.

8.6. Kamati ya Mazingira itaandika taarifa yake ya utekelezaji mara moja kwa mwezi kwa Afisa Mtendaji wa Kijiji ambaye atawajibika kutoa taarifa hizo kwenye vikao vya Halmashauri ya kijiji kila mwezi na Mkutano Mkuu wa kijiji mara nne kwa mwaka yenye nakala kwa Afisa Misitu (W) mara nne kwa mwaka.

8.7. Iwapo kutakuwa na malalamiko yoyote kuhusu Kamati ya Mazingira ni lazima Mwenyekiti au Afisa Mtendaji wa Kijiji achunguze malalamiko hayo kwa kushirikisha wajumbe wa Halmashauri ya kijiji na kuchukua hatua zinazostahili kurekebisha dosari zinazolalamikiwa iwapo zitathibitika.

## 9. Majukumu ya Kamati ya Mazingira

9.1. Kamati ya Mazingira itakuwa na majukumu yafuatayo:

9.1.1. Kuhakikisha kuwa mipaka yote ya msitu wa hifadhi ya kijiji na hifadhi ya mazalia ya samaki ya Ziwa Tanganyika sehemu ya Kashagulu inaeleweka waziwazi kwa wanakijiji wote wa Kashagulu.

9.1.2. Kusimamia utekelezaji wa mipango yote inayohusu utumiaji, ulinzi na uendelezaji wa msitu na mazalia ya samaki ya Ziwa Tanganyika sehemu ya kijiji cha Kashagulu.

9.1.3. Kwa kushirikiana na Halmashauri ya kijiji na wanakijiji wengine kutambua na kutenga msitu katika kanda / maeneo mbalimbali (matumizi /uhifadhi) kulingana na hali halisi ya msitu.

9.1.4. Kutunza kumbukumbu zote zinazohusu shughuli za utumiaji, ulinzi, na uendelezaji wa msitu wa hifadhi ya kijiji. Kumbukumbu hizo ni:-

- 9.1.4.1 Mihtasari ya mikutano
- 9.1.4.2 Doria
- 9.1.4.3 Uhalifu na faini
- 9.1.4.4 Vibali vilivyotolewa
- 9.1.4.5 Mapato na matumizi ya fedha za msitu na hifadhi ya mazalia ya samaki ya Ziwa Tangnyika
- 9.1.4.6 Uoteshaji na upandaji miti, pia shughuli zote za uhifadhi mazingira ndani ya maeneo ya kijiji

9.1.5. Kuhakikisha kuwa walinzi wa msitu na hifadhi ya mazalia ya samaki wanatekeleza kazi yao kikamilifu na kuchukua hatua zinazopasa kuondoa dosari zinazojitokeza katika kazi ya ulinzi.

9.1.6. Kufanya ukaguzi wa msitu wa hifadhi na hifadhi ya mazalia ya samaki ya kijiji angalau mara mbili kwa mwezi.

9.1.7. Kuhakikisha matumizi endelevu ya msitu na Ziwa Tanganyika yanazingatiwa kulingana na kanuni za matumizi zilizowekwa na kukubaliwa.

9.1.8. Kuwashughulikia wahalifu wa msitu na Ziwa Tanganyika kwa mujibu wa kanuni za adhabu

zilizowekwa na kukubalika kwa ushirikiano na Halmasahauri ya kijiji.

9.1.9. Kwa ushirikiano na Halmashauri ya kijiji, kuwahamasisha wanakiiji kushiriki katika suala zima la uhifadhi wa msitu, Ziwa Tanganyika na mazingira ya kijiji kwa ujumla.

9.1.10. Kutumia na kutunza vitabu vya stakabadhi vilivyoidhinishwa na Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma.

9.1.11. Kufungua Akaunti Benki ya Kamati ya Mazingira ya kijiji kwa ajili ya kuweka fedha za mapato ya msitu na hifadhi ya mazalia ya samaki ya Ziwa Tanganyika (ushuru na faini).

9.1.12. Kuhakikisha kuwa fedha za Akaunti ya Kamati ya Mazingira zinatumika kama zilivyokusudiwa na kuidhinishwa na Halmashauri ya kijiji cha Kashagulu.

9.1.13. Kuweka utaratibu wa utoaji wa vibali ili kuhakikisha kuwa vibali vinavyotolewa ni vile vilivyoko katika mamlaka ya Kamati ya Mazingira na kwamba utoaji wa vibali unakwenda sambamba na mahitaji yaliyopo na sio vinginevyo.

## 10. Ulinzi na Ukaguzi wa Msitu wa Hifadhi ya kijiji na Hifadhi ya Mazalia ya Samaki ya Ziwa Tanganyika Sehemu ya Kijiji cha Kashagulu

10.1. Kila mwanakijiji wa Kashagulu ana jukumu la kulinda na kutunza hifadhi ya ziwa na msitu wa kijiji. Hili jukumu litafanyika kwa kutekeleza yafuatayo:

10.1.1. Kutoa taarifa za uhalifu

10.1.2. Kutambua na kutoa taarifa za wahalifu wa msitu na Ziwa Tanganyika, na zana zao haramu.

10.1.3. Kuzuia moto usitokee na kuzima unapotokea.

10.1.4. Kushiriki katika shughuli za uoteshaji miche ya miti na upandaji wa miti.

10.1.5. Wakazi wa kijiji ambao maeneo yao yanapakana na msitu wa hifadhi ya kijiji na hifadhi ya mazalia ya samaki ya Ziwa Tanganyika sehemu ya Kashagulu wana wajibu wa ziada wa kuhakikisha kuwa eneo hilo haliingiliwi na kuharibiwa kwa namna yeyote ile.

10.1.6. Ni wajibu wa wakazi wote wa kijiji cha Kashagulu kushirikiana katika ulinzi wa msitu wa hifadhi ya kijijii na hifadhi ya mazalia ya samaki ya Ziwa Tanganyika sehemu ya kijiji cha Kashagulu.

**11. Walinzi wa Msitu wa hifadhi ya kijiji na Hifadhi ya Mazalia ya Samaki ya Ziwa Tanganyika**

11.1. Doria za ukaguzi katika msitu wa hifadhi ya kijiji na hifadhi ya mazalia ya samaki ya Ziwa Tanganyika sehemu ya kijiji cha Kashagulu zitafanywa na walinzi/wanadoria angalau mara tatu kwa wiki.

11.2. Walinzi wa msitu na hifadhi ya mazalia ya samaki ya Ziwa Tanganyika watachaguliwa na Halmashauri ya kijiji na kuthibitishwa na Mkutano Mkuu wa kijiji kutoka katika vitongoji vyote vya kijiji na idadi yao haitakuwa chini ya wajumbe kumi (10). Vitongoji vya Ugalaba, Ubanda na Lufubu vitatoa walinzi wawili kila kitongoji na vitongoji vingine vitatoa mmoja kila kitongoji.

11.3. Walinzi wa msitu na hifadhi ya mazalia ya samaki ya Ziwa Tanganyika watakaochaguliwa wanatakiwa kuwa na tabia zifuatazo:

11.3.1. Awe na tabia na mwenendo mzuri.

11.3.2. Wenye kujituma na mwaminifu.

11.3.3. Mkakamavu na mwenye afya nzuri.

11.3.4. Asiwe mlevi

11.3.5. Awe mkazi wa kijiji cha Kashagulu na raia wa Tanzania.

11.3.6. Awe na umri wa miaka kumi na nane (18) na kuendelea

11.4. Walinzi watachagua kiongozi wao (Kamanda) kutoka miongoni mwao ambaye atawajibika kupanga utaratibu wa doria kwa kushirikiana na wanadoria wengine na utoaji taarifa kwa Kamati ya Mazingira.

11.5. Walinzi wa msitu na hifadhi ya mazalia ya samaki ya Ziwa Tanganyika hawatalipwa mishahara lakini watapata motisha kama itakavyoamuliwa na serikali ya kijiji. Aidha walinzi husika wanaweza kupewa 30% ya faini anayotozwa mhalifu. Vile vile walinzi wa msitu wa hifadhi ya kijiji na mazalia ya samaki ya Ziwa Tanganyika wanaweza kusamehewa kazi nyingine za maendeleo kijijini.

11.6. Mwenyekiti wa vi/kitongoji kinachopakana na msitu wa hifadhi ya kijiji na hifadhi ya mazalia ya samaki ya Ziwa Tanganyika sehemu ya kijiji cha Kashagulu anao wajibu wa kuhakikisha kuwa ulinzi wa msitu wa hifadhi ya kijiji na mazalia ya samaki unafanyika ipasavyo kwa kushirikiana na walinzi na wanakitongoji wake.

11.7. Afisa Mtendaji wa Kata anao wajibu wa kutoa msukumo katika ulinzi wa msitu wa hifadhi wa kijiji na hifadhi ya mazalia ya samaki ya Ziwa Tanganyika katika Kata yake.

11.8. Afisa Misitu/Uvuvi/Nyuki/Wanyamapori (W) anao wajibu wa kukagua maeneo ya msitu wa hifadhi ya kijiji na hifadhi ya mazalia ya samaki ya Ziwa Tanganyika sehemu ya Kashagulu wakati wowote na kusaidia kazi ya ulinzi pale inapohitajika kufanya hivyo.

**12. Masharti ya Kuingia msitu wa Hifadhi ya Kijiji na Hifadhi ya Mazalia ya Samaki ya Ziwa Tanganyika Sehemu ya Kashagulu.**

12.1. Mkazi yeyote wa kijiji cha Kashagulu, Afisa Misitu/Uvuvi au mtu yeyote aliyeruhusiwa wanaweza kuingia msitu wa hifadhi ya kijiji na hifadhi ya mazalia ya samaki ya Ziwa Tanganyika sehemu ya Kashagulu.

12.2. Afisa Misitu/Uvuvi/Nyuki/Wanyamapori yeyote wa Idara ya Misitu na Nyuki, Wanyamapori na Uvuvi wakati wowote anaweza kuingia ndani ya msitu wa hifadhi ya kijiji na hifadhi ya mazalia ya samaki ya Ziwa Tanganyika sehemu ya Kashagulu aidha akiwa peke yake au kwa kushirikiana na Kamati ya Mazingira ya kijiji kwa lengo la kufanya ukaguzi na kutoa ushauri kwa Kamati ya Mazingira ambao unapaswa kupokelewa na kufanyiwa kazi kwa lengo la kuboresha uendelezaji wa eneo hilo la msitu/ziwa.

12.3. Sio ruksa kwa mtu yeyote kuingia msitu wa hifadhi ya kijiji na hifadhi ya mazalia ya samaki ya Ziwa Tanganyika sehemu ya Kashagulu bila kibali kutoka

kwa Kamati ya Mazingira isipokuwa walinzi wa msitu, Kamati ya Mazingira, Halmashauri ya kijiji na Afisa Misitu/Uvuvi wanaweza kufanya hivyo bila kibali.

12.4. Wageni wote wenye vibali toka Wizarani, Wilayani au wafadhili ni sharti wapite kijijini na kuonyesha vibali vyao kwa Kamati ya Mazingira ya kijiji kabla ya kuanza kufanya kazi yoyote ndani ya msitu wa hifadhi au hifadhi ya mazalia ya samaki ya Ziwa Tanganyika sehemu ya kijiji cha Kashagulu.

## 13. Masharti ya Matumizi ya Msitu wa Hifadhi ya Kijiji na Hifadhi ya Mazalia ya Samaki ya Ziwa Tanganyika sehemu ya Kashagulu.

13.1. Mahitaji yote yanayohusu ukataji miti aina fulani kwa ajili ya mbao, nguzo na miamba ya nyumba ndani ya msitu wa hifadhi ya kijiji cha Kashagulu yanaruhusiwa katika **Ukanda wa Bubaja** na **Mbebhe kwa kibali** kitakachotolewa na Kamati ya Mazingira ya kijiji. Mbaozitagongwa alama (nyundo) itakayotolewa na **Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma** kama ilivyoainishwa katika Mpango wa Usimamizi Shirikishi wa Msitu wa Hifadhi ya kijiji. Miti husika itavunwa kwa kiwango ambacho hakitaathiri lengo la msingi la kuhifadhi msitu ambalo ni kuhifadhi vyanzo vya maji na uendelevu wa rasilimali na huduma ya msitu kwa vizazi vya sasa na vijavyo vya Tanzania na ulimwengu kwa jumla. Miti aina ya Mninga, Mpilipili, Mzingati, Mkoma, Mkamba na Mkola haitaruhusiwa kuvunwa ndani ya maeneo ya matumizi.

## 14. Vitendo Vilivyopigwa Marufuku

14.1. Vitendo vifuatavyo vimepigwa marufuku kufanyika katika msitu wa hifadhi ya kijiji na hifadhi ya mazalia ya samaki ya Ziwa Tanganyika sehemu ya Kashagulu:

14.1.1 Kuchoma moto msitu.

14.1.2 Kuchungia mifugo (ng'ombe, mbuzi, kondoo, punda, n.k) msituni.

14.1.3 Kukata miti au uoto wa asili kwenye vyanzo vya maji, miteremko mikali na makorongo.

14.1.4 Kuwinda asali (Kukata miti yenye pango ambayo kuna nyuki)

14.1.5 Kuingilia eneo la msitu na kingo za Ziwa Tanganyika kwa kilimo na makazi.

14.1.6 Kutengeneza mkaa.

14.1.7 Kukata/kutoa magome miti mibichi kwa ajili ya kuni (matumizi ya biashara na nyumbani).

14.1.8 Uwindaji wa wanyamapori katika msitu wa hifadhi ya kijiji kwa kutumia bunduki, mshale, mbwa na mitego (waya au kamba).

14.1.9 Kupasua mbao miti aina ya Mninga, Mzingati, Mpilipili, Mkoma, Mkamba na Mkola kwa kuwa ni michanga.

14.1.10 Kuvua samaki ndani ya Ziwa Tanganyika kwa kutumia zana haramu kama vile kokoro (mkwabho), nyavu za macho madogo chini ya kalamu ya bic, makila chini ya inchi tatu (3), katuli, kutumia sumu na baruti.

14.1.11 Kuvua samaki kwa kutumia zana yoyote ile ndani ya hifadhi ya mazalia ya samaki ya Ziwa Tanganyika

## 15. Vitendo Vinavyoruhusiwa kwa Vibali na Malipo

15.1. Vitendo vifuatavyo vinaweza kufanyika kwenye msitu wa hifadhi ya kijiji cha Kashagulu kwa kibali na malipo:

15.1.1 Kupasua mbao aina husika ya miti katika Ukanda wa Bubaja na Mbebhe.

15.1.2 Kukata miti ya ujenzi – nguzo na miamba ya Mkurungu, Mhongolo na Msongati

15.1.3 Kukata mianzi kwa matumizi ya nyumbani na biashara.

15.1.4 Kukata ukindu kwa matumizi ya nyumbani na biashara

15.1.5 Kuchuma dawa za asili ndani ya msitu wa hifadhi ya kijiji kwa watu toka nje ya kijiji cha Kashagulu.

15.1.6 Utengenezaji wa nyungo na vitunga kutokana na mianzi.

15.1.7 Wageni kutembelea msitu wa hifadhi ya kijiji na hifadhi ya mazalia ya samaki ya Ziwa Tanganyika sehemu ya kijiji cha Kashagulu kwa dhumuni la utalii, Ziara za mafunzo na watafiti.

15.1.8 Kukata mipini kwa ajili ya biashara tu.

15.1.9 Kukata kamba kwa ajili ya biashara.

15.1.10 Kuuza mbegu za Myovu kwa Wakala wa Mbegu za Miti Tanzania.

15.1.11 Uwekezaji wa aina yoyote ile ndani ya msitu wa hifadhi ya kijiji na hifadhi ya mazalia ya samaki ya Ziwa Tanganyika sehemu ya kijiji cha Kashagulu <u>utalipiwa</u> kufuatana na thamani ya mtaji na kusainiwa kwa <u>Mkataba wa Makubaliano.</u>

15.2. Kibali cha kuruhusu vitendo vilivyotajwa kitatolewa baada ya maombi ya mhusika kupokelewa na

kujadiliwa na Kamati ya Mazingira na kuridhika kwamba mazao au huduma hizo zinaweza kupatikana bila kuleta athari kwa eneo husika la msitu au Ziwa Tanganyika. Kibali kitaonyesha kiasi cha mazao, tarehe ya mwisho na malipo yaliyofanyika.

## 16. Kiasi cha malipo

16.1. Kiasi cha malipo kitakuwa kama ilivyoelezwa kwenye kiambatanisho Jedwali 1:

| **Aina ya mazao/huduma ya Msitu na Ziwa** | **Kiasi/Idadi** | **Malipo (Tshs)** |
|---|---|---|
| Nguzo/Mwamba wa nyumba | 1 | 100 |
| Mianzi kwa matumizi ya nyumbani na biashara | 1 | 50 |
| Kutengeneza nyungo kutokana na mianzi | 1 | 50 |
| Kuchuma dawa za asili ndani ya msitu wa hifadhi ya kijiji | Kila aina ya mti/mmea | 1,000 |
| Mbao | 1 | 300 |
| Mpini kwa ajili ya biashara | 1 | 100 |
| Ukindu kwa matumizi ya nyumbani na biashara | 1 fungu | 50 |
| Ziara za mafunzo:<br>▪ Watanzania | Kikundi kwa siku | 15,000 |
| ▪ Toka nchi za nje | Kikundi kwa siku | 30,000 |
| Watalii:<br>▪ Watanzania | 1 kwa siku | 1,000 |
| ▪ Toka nje- wenye vibali vya kufanya kazi nchini | 1 kwa siku | 3,000 |

| Aina ya mazao/huduma ya Msitu na Ziwa | Kiasi/Idadi | Malipo (Tshs) |
|---|---|---|
| ▪ Toka nje wasiokuwa na vibali vya kufanya kazi nchini | 1 kwa siku | 5,000 |
| Watafiti<br>▪ Wanafunzi vyuo vya elimu ya juu | 1 kwa siku | 500 |
| ▪ Toka nje ya nchi | 1 kwa siku | 1,000 |
| ▪ Wahadhiri Watanzania | 1 kwa siku | 1,000 |
| Kamba za miti ya miyombo kwa matumizi ya nyumbani na biashara | 1 fungu (puli) | 50 |
| Mbegu za Myovu | Mapato yote kwa mkusanyaji | 10% |
| Uwekezaji ndani ya msitu | Thamani ya mtaji na Mkataba wa Makubaliano | |

## 17. Vitendo Vinavyohitaji Kibali bila malipo (Bure)

17.1. Vitendo vifuatavyo vitaruhusiwa kufanyika kwenye msitu wa hifadhi ya kijiji na hifadhi ya mazalia ya samaki ya Ziwa Tanganyika sehemu ya kijiji cha Kashagulu kwa kibali/ruhusa kisicholipiwa (bure):-

17.1.1. Kutumia maji kwa matumizi ya nyumbani, mifugo na kilimo.

17.1.2. Kuokota kuni kavu kwa matumizi ya nyumbani na biashara.

17.1.3. Kukata fimbo za kutembelea.

17.1.4. Kuchukua mboga, uyoga na matunda.

17.1.5. Kuchonga mwiko kwa ajili ya matumizi ya nyumbani na biashara.

17.1.6. Kuchukua udongo dawa kwa ajili ya ukindu na nyungo

17.1.7. Kufanya matambiko na ibada.

17.1.8. Ziara za mafunzo kwa ajili ya wanafunzi Watanzania wa shule za awali, msingi, sekondari na vyuo visivyo vya elimu ya juu

17.1.9. Kuchuma dawa za asili kwa njia endelevu

17.1.10. Njia za usafiri kwa miguu na gari (Kashagulu kwenda Mwese na Rukoma)

17.1.11. Kuchukua nyasi za kuezekea nyumba.

17.1.12. Kutundika mizinga ya nyuki.

17.1.13. Kukata kamba kwa ajili ya matumizi ya nyumbani.

17.1.14. Kukata mianzi, nguzo na miamba ya nyumba kwa kaya ambayo imepata matatizo kama vile ya kuunguliwa moto nyumba.

## 18. Viwango vya Faini

18.1. Mtu yeyote akikiuka sheria hii atakuwa ametenda kosa na akithibitika atatozwa faini isiyopungua shilingi elfu ishirini (20,000/=) na isiyozidi shilingi elfu hamsini (50,000/=).

18.2. Iwapo kosa lililofanyika litahusu, vitendo vilivyopigwa marufuku 13(1) mhalifu/mkosaji atatozwa faini isiyopungua elfu arobaini na tano (Tshs. 45,000/=) na isiyozidi shilingi elfu hamsini (Tshs. 50,000/=) kwa kila kosa pamoja na fidia kutokana na tathimini ya Afisa misitu wa eneo/ Wilaya husika kwa kila kosa kulingana na kiwango cha uharibifu. Pia mhalifu atafidia gharama za ukamataji (mgambo). Kwa mtu kukataa kushiriki katika kuzima moto ndani ya msitu wa hifadhi ya kijiji cha Kashagulu, faini na adhabu zilizotajwa hapo juu zitatumika pia.

18.3. Kwa mtu/watu kuzuia Kamati ya Mazingira kufanya kazi yake barabara, kama vile vitisho kwa

wanakamati ya mazingira viwango vya faini vilivyotajwa hapo juu (Tshs 45,000 – 50,000/=) vitatumika kwa kila mhusika.

18.4. Iwapo kosa lililotendwa litahusu vitendo vinavyohitaji kibali na malipo 14(1) basi mkosaji / mhalifu atatozwa faini isiyopungua fedha za kitanzania elfu ishirini (Tshs 20,000/=) na isiyozidi elfu arobaini (Tshs 40,000/=) pamoja na fidia ya mazao yaliyoharibiwa na gharama zitakazojitokeza.

18.5. Iwapo kosa lililotendwa litahusu vitendo vinavyoruhusiwa kufanyika kwa kibali kisicholipiwa 17.1. (bure) basi Kamati ya Mazingira italiangalia hilo kulingana na ukubwa wa kosa. Kwa makosa kama haya mhalifu atazuiliwa kupata huduma hiyo kwa muda wa miezi sita (6). Hata hivyo katika kuamua makosa katika kundi hili lazima Afisa misitu wa eneo / Wilaya husika ashirikishwe kama yuko karibu.

18.6. Kwa makosa yatakayohusu uchungiaji mifugo (mbuzi, ng'ombe, kondoo na nguruwe), faini itakuwa Tshs 2000/= (elfu mbili) kwa kila mnyama. Faini hii itatumika mara mbili tu kwa mkosaji, yaani kama mhusika atafanya makosa kuchungia mifugo msituni mara mbili, zaidi ya hapo yaani mara ya tatu basi mifugo itataifishwa kwa kutumia Sheria ya Misitu No. 14, 2002.

18.7. Kama mhalifu atakuwa amekiri kosa na hana uwezo wa kulipa faini na Kamati ya Mazingira ikaridhika, basi mtu huyo anaweza kupewa kazi za mikono kama vile kufyeka mpaka, n.k. kwa makosa yale yatakayoangukia katika kifungu cha 17 (1).

**19. Gharama na Fidia**

19.1. Kamati ya Mazingira inaweza kutoza gharama nyingine mbali na faini na fidia za uharibifu, kama vile gharama za ukamataji na kushughulikia wahalifu. Gharama hizi zitawekwa kufuatana na kila kosa lililotendwa; kwa mujibu wa Sheria Na. 7 ya 1982 kifungu cha 16 (2), (3) ya Sheria za Serkali za Mitaa.

**20. Faini ya wenye Dhamana/ Madaraka**

20.1. Iwapo mjumbe yeyote katika Halmashauri ya Kijiji, Kamati ya Mazingira au walinzi wa msitu na Ziwa Tanganyika atakiuka taratibu za kiutendaji kuhusiana na uhifadhi wa msitu wa hifadhi na hifadhi ya mazalia ya samaki ya Ziwa Tanganyika sehemu ya kijiji cha Kashagulu, atakuwa ametenda kosa kwa mujibu wa Sheria hii na atatozwa faini itakayojulikana kama faini ya wenye dhamana/ madaraka. Faini hiyo itakuwa mara mbili ya faini zitakazotozwa kwa watu wasiokuwa na madaraka kijijini/ zilizoainishwa hapo juu.

20.2. Pamoja na faini hizo, makosa ya viongozi hao lazima yajadiliwe kwenye vikao vya juu katika kijiji na kuwachukulia hatua kali kama vile barua za onyo la maandishi, kusimamishwa na kuwaondoa kwenye nafasi zao baada ya kuidhinishwa na Mkutano Mkuu wa Kijiji.

20.3. Kwa wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji, Afisa Mtendaji Kata ataitisha Kikao kujadili hatima ya kiongozi aliyefanya uhalifu huo.

**21. Taratibu za Kushughulikia Wahalifu wa Msitu wa Hifadhi na Hifadhi ya Mazalia ya Samaki ya Ziwa Tanganyika sehemu ya Kashagulu.**

21.1. Hairuhusiwi kwa mwanakijiji, mwanakamati ya Mazingira, mlinzi au kiongozi yeyote kumtoza faini mhalifu akiwa peke yake.

21.2. Mazao ya misitu na ziwa yaliyovunwa kinyume cha utaratibu pamoja na zana zilizotumika katika uhalifu huo yakikamatwa ni lazima yafikishwe kwenye ofisi ya kijiji ambapo hatua zaidi itachuliwa na Kamati ya Mazingira ya kijiji.

21.3. Iwapo itabainika kuwa mtu au watu wamekiuka taratibu za matumizi ya msitu wa hifadhi ya kijiji na hifadhi ya mazalia ya samaki ya Ziwa Tanganyika sehemu ya kijiji cha Kashagulu, mtu huyo au watu hao watafikishwa mbele ya Kamati ya Mazingira ya kijiji na suala lao litashughulikiwa kwa utaratibu ufuatao hapa chini:

21.3.1. Mhalifu/wahalifu watafikishwa katika ofisi ya kijiji ambapo Afisa Mtendaji wa Kijiji atamuweka/atawaweka chini ya ulinzi. Afisa Mtendaji wa Kijiji atawaarifu viongozi wa Kamati/wajumbe wa Kamati ya Mazingira angalau wawili ili kuwatoza faini wahalifu iwapo watakiri/atakiri kosa kwa kuweka sahihi katika daftari la“Makosa na Faini”.

21.3.2. Iwapo mhalifu/mtuhumiwa atakataa kukiri kutenda kosa kwa kukataa kuweka sahihi katika daftari, mtu huyo atatakiwa kupelekwa mahakamani.

21.3.3. Endapo mhalifu/wahalifu watakiri kutenda kosa, faini yote lazima iwe imelipwa katika muda wa siku tatu **(3)** toka siku ya kukiri kutenda kosa hilo. Hata hivyo mhalifu atalazimika kuwekewa dhamana na mtu anayekubalika katika kijiji cha Kashagulu.

21.3.4. Katibu atapokea malipo ya faini iliyolipwa kwa kuandika stakabadhi ambayo atampatia mhalifu. Namba ya stakabadhi iliyotolewa itaandikwa kwenye daftari la "Makosa na Faini" na kumkabidhi Mweka Hazina azipeleke kwenye akaunti ya Kamati ya Mazingira ya kijiji.

21.4. Iwapo mtu anayetuhumiwa kutenda kosa atakataa kukiri kosa mbele ya Kamati ya Mazingira na mbele ya Mwenyekiti wa Kijiji au Afisa Mtendji wa Kijiji basi itabidi vyombo hivyo vya utendaji vifikishe shauri hili mahakamani kwa uamuzi zaidi. Iwapo mhalifu atashindwa kulipa faini katika kipindi kilichokubaliwa basi Kamati ya Mazingira au Afisa Mtendaji wa Kijiji atafikisha suala hilo mahakamani.

21.5. Faini na /au adhabu nyingine zitatozwa kwa kuzingatia viwango vilivyowekwa, katika kifungu cha 18.1 – 18.7 ya Sheria hii.

21.6. Mashauri yatakayoshindikana kuamuliwa kijijini itabidi yafikishwa mahakamani na yasimamiwe na Afisa Misitu wa wilaya, Tarafa au Kata. Afisa Mtendaji wa kijiji na Kamati ya Mazingira watapaswa kuwa mashahidi katika kesi hiyo.

**22. Namna ya Kushughulikia Mazao ya Msitu na Ziwa Tanganyika Yaliyokamatwa, Faini Zilizotozwa na Mgawanyo Wake:**

22.1. Mazao ya msitu/ziwa yaliyovunwa kinyume cha Sheria pamoja na zana zilizotumika katika uhalifu huo vikikamatwa ni lazima vifikishwe kwenye ofisi ya kijiji ambapo hatua zaidi zitachukuliwa na Kamati ya Mazingira. Mapato kutokana na mauzo ya mazao ya msitu/ziwa yaliyokamatwa yatagawanywa kati ya Halmashauri ya kijiji 95% na Serikali Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma 5%, aidha zana zitachukuliwa na Halmashauri ya kijiji cha Kashagulu. (hazitagawanywa kati ya Halmashauri ya Wilaya na Halmashauri ya kijiji).

22.2. Mazao ya msitu yaliyokamatwa kwa ushirikiano wa kijiji na Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma mapato yatagawanywa kwa 50% kila mmoja.

22.3. Mazao ya msitu na Ziwa Tanganyika yaliyokamatwa na Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma peke yake kutokana na kijiji kuzembea, kijiji husika hakitapewa mgao wa mapato.Hata hivyo, Halmashauri ya kijiji itaadhibiwa kwa kutozwa faini ya asilimia 30% ya thamani ya mali iliyokamatwa au kushitakiwa kutokana na uzembe huo.

22.4. Thamani ya mazao ya msitu na Ziwa Tanganyika yakikamatwa na kijiji peke yake ni lazima mapato yagawanye kama 22(1) hapo juu kila mmoja.

22.5. Kama Mahakama itaamua kutumia Sheria kuu ya Misitu (Sheria Misitu 14, 2002) kifungu 89(1) na Sheria Kuu ya nchi kutoa maamuzi au adhabu basi Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma itakuwa

Mlalamikaji (Jamhuri) na Kamati ya Mazingira ya kijiji itakuwa ni Shahidi (informer), kwa hiyo faini itakayotozwa italipwa mahakamani, hivyo hakuna mgao wa faini hiyo.

22.6. Endapo kuna mazao ya misitu yatakayorudishwa wilayani (mlalamikaji), basi mapato yatagawanywa kama 22(1) hapo juu kati ya Halmashauri ya wilaya na Halmashauri ya Kijiji.

**23. Kuwasilisha Mashauri Mahakamani**

23.1. Iwapo mhalifu atashindwa kulipa faini katika kipindi kilichokubaliwa basi Kamati ya Mazingira na Afisa Mtendaji wa kijiji atafikisha suala hilo mahakamani

23.2. Iwapo mtu anayetuhumiwa kutenda kosa atakataa kukiri kosa mbele ya Kamati ya Mazingira na mbele ya Mwenyekiti wa kijiji au mbele ya Afisa Mtendaji wa Kijiji basi vyombo hivi vya utendaji vitawakilisha shauri hilo mahakamani kwa uamuzi zaidi.

23.3. Iwapo mhalifu atashindwa/kukataa kulipa faini suala hilo litafikishwa mahakamani

**24. Hatua za Mahakamani**

24.1. Katika kuendesha kesi, Mahakama itakuwa na haki ya kurejea kwenye Sheria ndogo za kijiji na wakati mwingine kuamua mhalifu kuadhibiwa kufuatana na Sheria hizo. Hii ni pamoja na faini, gharama za usumbufu, fidia za uharibifu zilipwe kwa Kamati ya Mazingira ya Kijiji cha Kashagulu.

24.2. Kama mahakama itatoa hukumu kufuatana na Sheria ya Misitu Na. 14 ya 2002, Kamati ya Mazingira ya Kijiji cha Kashagulu itakuwa kama

mtoa taarifa (informer) na itapata nusu ya faini atakayotozwa mhalifu chini ya kifungu cha 89(1) na fedha hizo zitawekwa kwenye Akaunti ya Kamati ya Mazingira ya kijiji cha Kashagulu.

**25. Mapato na Matumizi ya Fedha za Hifadhi ya Msitu na Hifadhi ya Mazalia ya Samaki ya Ziwa Tanganyika Sehemu ya Kijiji cha Kashagulu.**

25.1. Mapato ya Kamati ya Mazingira yatatokana na:

25.1.1. Faini zitakazotozwa wahalifu wa msitu na hifadhi ya mazalia ya samaki ya Ziwa Tanganyika.

25.1.2. Malipo ya mazao na huduma ya msitu wa hifadhi ya kijiji hifadhi ya mazalia ya samaki ya Ziwa Tanganyika yaliyoruhusiwa kwa kulipia katika Mpango huu.

25.1.3. Mauzo ya mbegu za miti aina ya Myovu (Mkangazi) kwa Wakala wa Mbegu za Miti Tanzania (Morogoro)

25.1.4. Mauzo ya mazao ya msitu na Ziwa Tanganyika yaliyokamatwa na zana zilizokamatwa katika ulinzi.

25.1.5. Wafadhili na wasamaria wema watakaotoa fedha/ msaada kwa ajili ya Usimamizi wa msitu wa hifadhi ya kijiji na hifadhi ya mazalia ya samaki ya Ziwa Tanganyika sehemu ya kijiji cha Kashagulu.

25.2. Mapato yatokanayo na mazao na huduma za msitu na Ziwa Tanganyika yatagawanywa kati ya Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma na kijiji cha Kashagulu kwa uwiano wa 95% Halmashauri ya kijiji na 5% kwa Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma.

25.3. Kijiji kitatakiwa kufungua Akaunti ya Benki kwa ajili ya kuhifadhi fedha za mapato hayo. Kamati ya Mazingira itahusika na ufunguaji wa akaunti hiyo.

25.4. Watakuwepo watia sahihi watatu kutoka ndani ya Kamati ya Mazingira. Fedha zinaweza kuchukuliwa Benki wakiwepo watia sahihi wawili (2), pamoja na Muhtasari wa kikao cha Kamati ya Mazingira kuonyesha Mpango wa Matumizi ya fedha husika ambao umeidhinishwa na Halmashauri ya kijij cha Kashagulu.

25.5. Mweka Hazina wa Kamati ya Mazingira atawajibika na upelekaji wa fedha za mapato Benki na uwekaji wa kumbukumbu katika daftari la fedha.

## 26. Matumizi ya Fedha za Kamati ya Mazingira

26.1. Matumizi ya fedha za akaunti ya Kamati ya Mazingira ni lazima yaidhinishwe na Halmashauri ya kijiji baada ya Kamati ya Mazingira kuomba kutumia fedha hizo kwa shughuli halali inayohusu maswala ya ulinzi na uendelezaji wa eneo la msitu wa kijiji na hifadhi ya mazalia ya samaki ya Ziwa Tanganyika sehemu ya Kashagulu.

26.2. Maombi ya Kamati ya Mazingira ya kutumia fedha sharti yaambatane na muhtasari wa kikao halali cha Kamati ya Mazingira chenye wajumbe wasiopungua nusu ya wajumbe wote kilichojadili maombi hayo ya matumizi ya fedha.

26.3. Matumizi ya fedha za Kamati ya Mazingira yanakusudiwa kuwa katika mambo yafuatayo:

26.3.1. Ununuzi wa vitabu vya kumbukumbu.

26.3.2. Ununuzi wa vitabu vya stakabadhi na hati ya malipo.

26.3.3. Kulipia gharama za kesi zinazohusu uharibifu wa msitu wa hifadhi ya kijiji, hifadhi ya mazalia ya samaki ya Ziwa Tanganyika na uharibifu wa mazingira mahakamani. Gharama hizi zitakuwa ni nauli, chakula na malazi ya mashahidi kwa viwango vitakavyoidhinishwa na Halmashauri ya kijiji.

26.3.4. Kugharamia shughuli za uoteshaji miche ya miti; kama viriba na mbegu.

26.3.5. Kulipia asilimia mia moja (100%) ya gharama za matibabu ya walinzi wa msitu walioumia kazini, baada ya kuthibitishwa na Kamati ya Mazingira.

26.3.6. Kutoa zawadi kwa walinzi waliofanya kazi nzuri kwa mwaka, kama itakavyopendekezwa na Kamati ya Mazingira na kuidhinishwa na Halmashauri ya Kijiji.

26.3.7. Kununua sare na kutengeneza vitambulisho kwa walinzi wa msitu.

26.3.8. Kutayarisha mabango ya kutoa onyo/ tahadhari kwa wananchi juu ya matumizi yasiyoruhusiwa ndani ya msitu wa hifadhi ya kijiji na hifadhi ya mazalia ya samaki ya Ziwa Tanganyika.

26.3.9. Kulipia gharama za mikutano, mafunzo na ziara za mafunzo kwa Kamati ya Mazingira, walinzi wa msitu na wanakijiji wengine kama itakavyoidhinishwa na Halmashauri ya kijiji cha Kashagulu.

26.3.10. Kutoa zawadi/motisha kwa wananchi wema watakaowezesha kutambua wahalifu wa

msitu, kukamatwa kwa wahalifu, kukamatwa kwa mazao ya msitu au yote pamoja. Zawadi kwa raia wema itakuwa asilimia kumi (10%) ya faini au thamani ya mazao ya msitu na hifadhi ya Ziwa Tanganyika yaliyokamatwa na kuuzwa kabla ya kugawanywa kati ya Halmashauri (W) na Halmashauri ya kijiji cha Kashagulu.

26.3.11. Kununua mahema na usafiri kwa ajili ya doria na ufuatiliaji wa utekelezaji wa“Mpango wa Usimamizi Shirikishi wa Msitu wa Hifadhi ya Kijiji na Hifadhi ya Mazalia ya Samaki ya Ziwa Tanganyika Sehemu ya Kashagulu”.

26.3.12. Kusaidia shughuli zingine za maendeleo kijijini endapo salio la Akaunti ya Kamati ya Mazingira litakuwa si chini ya Tshs **1,000,000/=** (shillingi milioni moja tu) kwa wakati huo na itakavyoidhinishwa na Halmashauri ya kijiji.

26.4. Taarifa ya mapato na matumizi ya fedha za Kamati ya Mazingira lazima itolewe na Afisa Mtendaji wa Kijiji katika Mkutano Mkuu wa kijiji mara nne (4) kwa mwaka yenye nakala kwa Afisa Misitu (W) husika.

25(4) Taarifa ya mapato na matumizi ya fedha za Kamati ya Mazingira lazima itolewe na Afisa Mtendaji wa Kijiji katika Mkutano Mkuu wa kijiji mara nne (4) kwa mwaka yenye nakala kwa Afisa Misitu (W) husika.

Uamuzi wa Mkutano Mkuu wa Kijiji cha Kashagulu wa tarehe....15/02/2010.... ulipitisha Sheria hii na kuthibitishwa na:

Sahihi ..................................

AFISA MTENDAJI WA KIJIJI ... ULU

Jina MAGRETH OBADIA

Afisa Mtendaji wa Kijiji
Kijiji cha Kashagulu

..................................

MWENYEKITI WA SERIKALI YA KIJIJI KASHAGULU, S.L.P 332, KIGOMA

MATWIGA SALUMU

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Kijiji
Kijiji cha Kashagulu

Muhuri wa Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma uliogongwa kufuatia azimio lililopitisha Sheria hii katika kikao cha Halmashauri ya Wilaya (Full Council) cha tarehe ..27/01/2020....na kuthibitishwa na:

Jina D.D.Z. Kuseka..................................

ALH. KASIMU NYAMUKUNGA..................................

Sahihi ..................................

Mkurugenzi wa Halmashauri (W)
Kigoma

MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA
KIGOMA

..................................

Mwenyekiti wa Halmashauri (W)
Kigoma

MWENYEKITI
HALMASHAURI YA WILAYA YA KIGOMA
S.L.P 332
KIGOMA